003

JARIBIO LA MTIHANI (EXCELLENT)

DARASA LA TANO - MWAKA 2014

KISWAHILI

Soma kifungu kifuatacho kisha ujaze nafasi kutoka1 - 15 kwa kuchagua jibu sahihi.

Alifunga safari yake___1___kwenda kijijini___2___ wanadamu. Alipita___3___mbuga na misitu na ___4___ mito yenye__5___ ya kutisha. Ilikuwa ni safari yenye ___6___ mengi mno. Wakati __7___jioni alipokuwa akijipumzisha, Bw. Kaguta_____8___ sauti __9___. Mbwa·alijificha na ___10___kwa makini. Mara akaona kiumbe ___11___ ajabu__-12___ kwa miguu ___13___ huku _____14_____ mti mrefu _____15___ haukuwa umechongwa. Begani mwake kilikuwa kimebeba paa aliyekuwa amemwua.

	A	B	C	D
1.	refu	ndefu	mrefu	ndevu
2.	cha	mwa	k wa	pa
3.	kwenye	penye	mwenye	yenye
4.	kufuka	kuvuka	kuruka	kupita
5.	mapango	maporomoko	miti	samaki
6.	uchovu	machovu	matatizo	taabu
7.	mmoja	moja	mwingi	mumoja
8.	aliskia	alisikiza	alisikia	alisikiliza
9.	geni	mgeni	zuri	ngeni
10.	kusikiliza	kusikiza	kusikizana	kusikilizana
11.	cha	wa	ya	kya
12.	kinatembea	kikitembea	akitembea	ametembea
13,	mawili	miwili	mbili	viwili
14.	amekamata	kimekamata	kilikamata	umekamata
15.	ambao	ambawo	ambaye	ambayo

Kutoka swai la 16 - 30, jibu kulingana na maagizo.

16. Kamilisha methali ifuatayo:
Mtaka yote hukosa_____
A. mwote B. pote C. yote D. chote

17. Neno kitabu kiko katika **NGELI** ya_____
A. LI - LI D. KI - VI
C. LI - YA D. A - WA

18. Ugonjwa wa kulala unaoambukizwa na mbung'o huitwa
A. malale B. majipu C. kichocho D. kifafa

19. Kamislisha sentensi hii:
Zizi ni _____ ya mifugo kama ng'ombe
A. makaazi B. chakula C. maji D. makazi

20. Wingi wa neno " jua" ni _____
A. kijijua B. majua C. vijijua D. jua

21. Taja umbo lililoonyeshwa hapa chini



A. mche duara
B. pia
C. mche
D. mraba

22. **Kamilisha tanakali ifuatayo:**
Wambui alianguka akalia_____
A. tititi B. Kwikwikwi C. uuui D. fofofo

23. Mtu anayetengeneza vyombo vya vyuma ni
A. sonara B. rubani C. mhunzi D. mwashi

24. Mmea uzaao ndizi huitwa
A. mgomba B. mndizi C. ndiziD. mdisi

25. Yupi si ndege wa nyumbani?
A. bata mzinga B. bata C. Kanga D. kuku

26. **Kamilisha kitendawili hiki:**
Namwosha mwanangu lakini hakauki_____
A. kichwa B. Ulimi C. moyo D. wayo

27. **Tumia kihusishi kujaza pengo:**
Gazeti lipo___ radio na rununu
A. jua ya B. Kando ya
C. kabla ya D. kati ya

28. Taja neno moja linalomaanisha orodha ya maneno uliyopewa:
Punda, nyati, fisi, ng'ombe, ngiri
A. wanyama B. mifugo
C. nyuni D. gagro

29. Sehemu iliyotiwa rangi huiteaje?

A. Robo
B. Sudusi
C. Robo mbili
D. Theluthi

30. Jaza pengo hili:
Kiti_____ni kizuri?
A. zipi B. kipi C. ipi D. lipi

Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali ya 31 - 40

Chura mdogo alikuwa kando ya bwawa la maji. Alikuwa akiota jua. Ng'ombe akaja kunywa maji yale. Chura mdogo alishangaa kumwona mnyama mkubwa kama yule.

Chura mdogo alikimbia akaenda kwa mama yake. Akamwambia mama yake, " mama, leo nimemwona mnyama mkubwa ajabu!" Mama chura hakujua ni mnyama gani anayesemwa. Naye hakujua kama kweli kuna mnyama mkubwa kumshinda. Akamwambia mtoto wake, " Hakuna mnyama mkubwa kuliko mimi!?

Mtoto wa chura alisema, "ni mkubwa kuliko wewe! nimnyama mkubwa kama mlima!"

Mama chura alivuta punzi nyingi akajivimbisha akawa mkubwa. Akamuuliza chura mdogo, " alikuwa mkubwa hivi?" " Hapana alikuwa mkubwa zaidi!" Chura mdogo alimwambia mama yake. Mama alivuta hewa akaingiza punzi nyingi zaidi. Akamwita mtoto wake amwangalie. Alivimbiza zaidi.

"Alikuwa mkubwa hivi?" mama alisema.

" Hapana, mama!La hasha! Alikuwa mkubwa kuliko hivyo! Mtoto wa chura alisema kwa sauti.

Mama alizidi kujikaza kwa nguvu zake zote. akajivimbisha mpaka akawa hwezi kupumua tena. Alipojaribu kusema, hakumaliza. Alipasuka pa! Akafa pale pale!.

31. Chura mdogo alikuwa kando ya bwawa akifanya nini?
    A. Akinywa maji B. Akicheza
    C. Akibarizi D. Akiota jua
32. Taja mnyama aaliyekuja kunywa maji_____
    A. ng'ombe B. chura C. Mama chura D. ndovu
33. Chura mdogo alimkimbilia nani?
    A. Ndovu B. Mama chura C. Ng'ombe D. Bwawa
34. " Hawezi kuwa mkubwa zaidi yangu!" Nani alisema maneno haya?
    A. Ng'ombe B. Mama chura
    C. Bwawa D. Maji
35. Ni viumbe vingapi vilivyotajwa katika hadithi hii?
    A. Wanne B. wawili C. Watatu D. Watano
36. Jina jingine la **Mama** ni _____
    A. mama chura B. abu C. shangazi D. nina
37. Mtoto wa chura alishangaa kwa nini?
    A. Kuona bwawa
    B. kuona ndovu
    C. Kumwona mama chura
    D. Kumwona mnyama mkubwa
38. Chura mdogo alimlinganisha ng'ombe na nini?
    A. Bwawa B. mama chura C. Mlima D. ndovu
39. Kwa nini mama alizidi kujikaza kuvimba?
    A. Afe B. Anenepe C. Ajivune D. Atishe
40. Ni nani aliyepasuka pa! Akafa?
    A. Mama chura B. Ng'ombe
    C. Mtoto wa chura D. Hatujui

Soma habari hii kisha ujibu maswali ya 41 - 50

Juzi tulikuwa mezani tukila mimi, ndugu zangu na wazazi wangu. Tukaamriwa tunawe mikono kwanza kabla ya kula. Haifai kula chakula kwa mikono michafu. Chakula kilitayarishwa na kuwekwa kwenye meza.Hata hivyo, baada ya kuketi kila mmoja kwenye kiti chake, hatukuanza kula tu kama inzi na paka, tulisali. Ilikuwa siku ya zamu yangu kusali. Baada ya sala tukapewa idhini ya kula.

Wazazi walitufundisha adabu njema ya kula. tuliambiwa kwamba wanyama ndio wanaokula bila ya kumshukuru **mwenyezi mungu**.

Bila baraka za Mungu, hakuna mlo. Yeye ndiye anayewalisha wanadamu na viumbe vyote. Ndiyo maana ni lazima kusali au kuomba kabla ya kula ili kumpa shukrani.

Tulikumbushwa kuwa si tabia njema kula haraka haraka kwa pupa kama nguruwe. Huo ni ulafi na ulafi ni tabia ya fisi. Wala si vizuri hata kidogo kujaza mafunda au matonge makubwa makubwa kinywani na kuanza kuongea kuonyesha watu chakula kilicho mdomoni. Haifai. Tabia njema ni kutia mdomoni chakula kiasi cha kutosha, kukitafuna, kisha umeze taratibu bila kusakamwa au kukabwa koo. Mwisho tuliambiwa kwamba, tukiwa mezani tusijaribu kusema, " **chakula ni kibaya.**"Kusema hivyo ni kumtukana mpish. Ni vibaya kusahau kumshururu na kumwambia asante mtu aliyepika. Hivyo ndivyo afanyavyo binadamu yeyote mwenye akili, busara na adabu njema.

41. Juzi tulikuwa nyumbani tukila na _____
    A. dada zangu B. wavyele wangu
    C. Jamaa yangu D. jirani zangu
42. Sote tulinawa mikono_____
    A. baada ya kula B. kabla ya wazazi
    C. baada ya wazazi D. kabla ya kuanza kula
43. Tulisali na kumwomba Mungu ili_____
    A. atupe chakula B. tushibe vizuri
    C. afurahi D. tumshukuru Mungu
44. Tabia ya kula haraka haraka kwa pupa huonyesha_____
    A. njaa B. fisi C. ulafi D. adabu
45. Jina jingine la mnyama ni _____
    A. chui B. hayawani C. ndovu D. kifaru
46. mnyama anayekula kwa pupa ni _____
    A. simba B. kondoo C. nguruwe D. fisi
47. Kamilisha methali hii:
    Haraka haraka haina_____
    A. baraka B. mwisho C. ujira D. haja
48. Jina jingine la Mungu ni _____
    A. Mola B. Sonara C. Mhunzi D. Seremala
49. Jaza: Mlafi kama_____
    A. nguruwe B. chui C. fisi D. chura
50. Taja jina jingine la **'mlo'**_____
    A. nyama B. mchuzi
    C. sebeho D. chukula

Powered by: Manyam Franchise
www.manyamfranchise.com

EXCELLENT EVALUATION TEST
STD. 5 MARKING SCHEME-2014

MATHS	ENGLISH	KISWAHILI	SCIENCE	SOCIAL STUDIES/C.R.E	
1.C	1.B	1.B	1.C	1.C	51.A
2.A	2.A	2.C	2.B	2.D	52.B
3.B	3.D	3.A	3.D	3.A	53.D
4.B	4.C	4.B	4.A	4.B	54.B
5.C	5.D	5.B	5.B	5.A	55.C
6.A	6.A	6.C	6.B	6.C	56.A
7.A	7.D	7.A	7.C	7.D	57.A
8.C	8.B	8.C	8.A	8.C	58.D
9.D	9.C	9.D	9.A	9.D	59.C
10.B	10.C	10.A	10.D	10.B	60.B
11.A	11.A	11.A	11.D	11.B	61.B
12.C	12.D	12.B	12.D	12.C	62.B
13.D	13.B	13.B	13.D	13.A	63.C
14.D	14.C	14.B	14.A	14.D	64.A
15.A	15.D	15.A	15.A	15.B	65.B
16.D	16.A	16.C	16.B	16.A	66.C
17.B	17.B	17.D	17.C	17.C	67.C
18.B	18.A	18.A	18.C	18.C	68.D
19.B	19.A	19.D	19.D	19.B	69.B
20.A	20.B	20.B	20.D	20.A	70.B
21.A	21.C	21.A	21.B	21.B	71.C
22.C	22.D	22.B	22.C	22.A	72.C
23.D	23.B	23.C	23.A	23.B	73.A
24.D	24.B	24.A	24.C	24.D	74.D
25.B	25.D	25.C	25.C	25.B	75.A
26.A	26.C	26.B	26.B	26.D	76.C
27.C	27.D	27.D	27.D	27.B	77.A
28.D	28.C	28.A	28.A	28.B	78.C
29.D	29.A	29.C	29.B	29.A	79.C
30.A	30.D	30.B	30.D	30.B	80.D
31.B	31.C	31.D	31.C	31.D	81.D
32.A	32.D	32.A	32.A	32.B	82.C
33.C	33.A	33.B	33.B	33.A	83.B
34.B	34.D	34.B	34.D	34.A	84.C
35.A	35.B	35.C	35.A	35.C	85.C
36.A	36.C	36.D	36.D	36.B	86.C
37.D	37.C	37.D	37.C	37.D	87.C
38.D	38.C	38.C	38.A	38. B	88.B
39.C	39.C	39.C	39.B	39.A	89.C
40.B	40.B	40.A	40.D	40.A	90.C
41.B	41.A	41.C	41.C	41.A	
42.A	42.C	42.D	42.B	42.C	
43.D	43.B	43.D	43.C	43.C	
44.A	44.D	44.C	44.D	44.D	
45.D	45.C	45.B	45.A	45.A	
46.A	46.C	46.D	46.A	46.C	
47.A	47.B	47.A	47.B	47.B	
48.D	48.B	48.A	48.C	48.C	
49.C	49.A	49.C	49.D	49.D	
	50.C	50.C	50.C	50.C	

Powered by:
anyam Franchise
www.manyamfranchise.com